**CHUO CHA USTAWI WA JAMII**

Dar es Salaam | Kilimanjaro



# JARIDA LA MTANDAONI

**Aprili - Juni, 2026**




Kaimu Mkurugenzi Kituo cha Maendeleo ya Teknolojia COSTECH Dkt. Erasto Mlyuka (watatu kushoto), Mwakilishi wa Mkuu wa Chuo ISW Dkt Riziki Nyello (wanne kushoto) wakimsikiliza Mwanafunzi wa ISW akiwasilisha wazo la ubunifu. Dar es Salaam, Aprili 21, 2026

# WANAFUNZI ISW WAONESHA UBUNIFU KWA VITENDO

**Na Mwandishi wetu**

KITUO cha ubunifu cha Chuo cha Ustawi wa Jamii , Aprili 21, 2026 kimeadhimisha siku ya kimataifa ya ubunifu na sanaa, ambapo wanafunzi wabunifu walionesha kazi zao za kibunifu mbele ya mgeni rasmi, Kaimu Mkurugenzi Kituo cha Maendeleo ya Teknolojia kutoka COSTECH Dkt. Erasto Mlyuka.

Akizungumza na wanafunzi wabunifu, Dkt. Mlyuka amesisitiza urasimishaji wa mawazo ya kibunifu ili kutambulika kibiashara na kuleta tija kwa wabunifu.
Amesema: "Ni vyema katika hatua hizi za awali kusajili kazi zenu katika mamlaka za usajili wa kazi za kisanii na haki miliki ili kuwanufaisha."

Dkt. Mlyuka ameongeza kuwa ni muhimu zaidi kupeleka bunifu hizi kwa walaji wa mwisho ili kufanyika majaribio kabla ya kumaliza kutengenza mifumo hii ya kidijitali na kuipeleka sokoni.

Aidha, amepongeza Chuo cha Ustawi wa Jamii kwa utayari na utashi wake wa hali ya juu kukuza na kuendeleza ubunifu na talanta za wanafunzi kupitia kituo cha ubunifu.

Kwa Upande wake, Mwakilishi wa Mkuu wa ISW, Dkt. Riziki Nyello amesema wanafunzi wahitimu wa chuo hicho ni bora zaidi kwenye soko la ajira kwa kuwa kinawapa nafasi kubwa kujifunza zaidi nje ya masomo ya kawaida ya darasani kwa vitendo kupitia programu mbali mbali ikiwemo kituo cha ubunifu.

Dkt. Nyello amepokea zawadi ya tuzo kwa niaba ya Dkt. Joyce Nyoni aliyotunukiwa na wanafunzi wa kituo cha ubunifu cha chuo wakitambua mchango wake wa kuwawezesha na kukuza bunifu zao na kufikia hatua za kutengeneza mifumo ya bunifu tayari kujaribiwa na kupelekwa sokoni baada ya kupata vibali vya mamlaka husika.



Mshauri Mkuu wa Kiufundi kutoka ILO-Tanzania Bi Aida Awel akiwasilisha mada katika mhadhara wa umma wenye lengo la kuwajengea uelewa Wanafunzi kuhusu changamoto za uhamiaji wa nguvu kazi na ushiriki wa vijana katika uhamiaji salama, Dar es Salaam, Juni 12, 2026.

# MHADHARA KUJENGA UELEWA WA UHAMIAJI WAFANYIKA ISW

**Na Mwandishi wetu**

TAASISI ya Ustawi wa Jamii (ISW), kupitia Idara ya Taaluma za Kazi kwa ushirikiano na Shirika la Kazi Duniani (ILO), imefanya mhadhara wa umma uliolenga kuwajengea uelewa wanafunzi kuhusu changamoto za uhamiaji wa nguvu kazi na ushiriki wa vijana katika uhamiaji salama.

Mhadhara huo wa kitaaluma uliofanyika Juni 12, 2026 chuoni hapo, uliongozwa na kaulimbiu ya "Tanzania Labour Migration Framework and Youth Engagement in Safe Migration." (Mfumo wa Tanzania wa Uhamaji wa Wafanyakazi na Ushiriki wa Vijana katika Uhamaji Salama wa Kikazi).

Lengo kuu la mhadhara huo lilikuwa ni kutoa uelewa mpana kwa wanafunzi juu ya changamoto mbalimbali zinazohusiana na uhamiaji wa wafanyakazi na kuwaelewesha sababu zinazowafanya watu wengi kukimbilia nje ya nchi kutafuta ajira.

Aidha, mkusanyiko huo ulikusudia kuwahamasisha na kuwandaa wanafunzi kushiriki kikamilifu katika kampeni za uhamiaji salama (safe migration) pamoja na kuwa mabalozi wa kutoa elimu na taarifa sahihi kwa jamii inayowazunguka ili kuepuka majanga kama usafirishaji haramu wa binadamu.

Mhadhara huo ulitawaliwa na mijadala ya kina iliyowezeshwa na wataalamu wabobezi kutoka ILO-Tanzania, wakiongozwa na Mshauri Mkuu wa Kiufundi, Aida Awel, Mratibu wa Kitaifa wa Mradi, Diana Rutrchura), pamoja na Ofisa Mawasiliano wa Kitaifa/National Communication Officer, Yonas Zewdie.

Wataalamu hao walichambua kwa kina mifumo ya kisheria na kisera inayolinda haki za wafanyakazi wanaohama, na namna vijana wanavyoweza kutumia fursa za kikanda kwa njia salama na halali.

“Tukio hili lilikuwa na umuhimu mkubwa sana kwa wanafunzi wa Chuo cha Ustawi wa Jamii, kwani limewapa fursa ya nadharia kukutana na vitendo kwa kujifunza moja kwa moja kutoka kwa wataalamu wa mashirika ya kimataifa,”amesema Mkuu wa Idara ya Taaluma za Kazi na Menejimenti ya Umma, Dkt. Jumanne Gomera.

Amesema mhadhara huo umewapa zana muhimu kiustawi zitakazowawezesha kuja kusaidia kutatua migogoro ya kikazi, kulinda haki za wafanyakazi, na kuishauri jamii pamoja na serikali kuhusu usimamizi bora wa rasilimali watu na ustawi wa jamii kwa ujumla.

Kwa mujibu wa Dkt. Gomera, ushirikiano kati ya ISW na ILO unaashiria hatua kubwa katika kuwaandaa wataalamu wa kesho wa masuala ya kazi nchini Tanzania, na kwamba kupitia elimu hii, wanafunzi sasa wapo katika nafasi nzuri zaidi ya kuwa mstari wa mbele kupambana na changamoto za ajira na uhamiaji usio salama, huku wakichochea mabadiliko chanya ya kisera na kijamii nchini.

---

## REHEMA SAID APEWA TUZO



Pichani ni Mkuu wa Chuo ISW, Dkt. Joyce Nyoni (kuli akimkabidhi Tuzo Mwanafunzi Rehema Said. (Kushoto) Naibu Mkuu wa Taasisi Fedha na Mipango Dkt. Zena Mabey Dar es Salaam, Mei 15, 2026.

**Na Mwandishi wetu**

MENEJIMENTI ya Chuo cha Ustawi wa Jamii (ISW) imempa tuzo maalum ya kutambua jitihada na kazi kubwa anayofanya mwanafunzi, Rehema Said kuipeperusha bendera ya nchi na ISW katika michuano ya kitaifa na kimataifa ya mchezo wa tennis (Wheelchair) ambapo tangu mwaka 2020 ameibuka mshindi wa tuzo mbali mbali Afrika na Duniani.

Mkuu wa Chuo cha Ustawi wa jamii Dkt. Joyce Nyoni amemkabidhi tuzo hiyo Mei 15, 2026 katika hafla ya kuwapongeza watumishi wa ISW waliofanya vizuri mwaka 2025.

---

## MENEJIMENTI YA ISW WATEMBELEA AUSTRIA



Mkuu wa Chuo ISW, Dkt. Joyce Nyoni (katikati) akiwa na Wahadhiri Waandamizi wakiwa The Management Centre Innsbruck nchini Austria. Mei 26, 2026.

**Na Mwandishi wetu**

Wahadhiri Waandamizi wa Taasisi ya Ustawi wa Jamii (ISW), wakiongozwa na Mkuu wa Taasisi hiyo, Dkt. Joyce Nyoni, wametembelea taasisi washirika ya The Management Centre Innsbruck ya nchini Austria. Ziara hiyo ni sehemu ya mradi wa utafiti wa pamoja unaochunguza mchango wa taaluma ya ustawi wa jamii katika kufikia Malengo ya Maendeleo Endelevu.

---

## ISW YAZINDUA VIMBWETA VIPYA




Mkuu wa Chuo ISW, Dkt. Joyce Nyoni, Mshauri wa Wanafunzi Dkt. Andrew Randa (kulia) pamoja na rais wa serikali ya wanafunzi 2025/26 Abdallah Zidane(katikati) katika uzinduzi wa vimbweta vipya. Dar es Salaam, Aprili 20, 2026.

**Na Mwandishi wetu**

MKUU wa Chuo cha Ustawi wa Jamii, Dkt. Joyce Nyoni, amezindua vimbweta vipya vilivyojengwa na serikali ya wanafunzi ya mwaka 2025/2026 chini ya uongozi wa rais Zidane Abdallah, ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa mradi wa maendeleo chuoni.



Mkuu wa Chuo ISW, Dkt. Joyce Nyoni pamoja na rais wa serikali ya wanafunzi 2025/26 Abdallah Zidane wakikata utepe ikiwa ni ishara ya kuzindua vimbweta vipya. Dar es Salaam, Aprili 20, 2026.

**Akizungumza katika uzinduzi, Dkt. Nyoni ameipongeza serikali ya wanafunzi kwa juhudi zao za kusimamia vyema rasilimali za wanafunzi kupitia michango na kufanikisha ujenzi wa vimbweta hivyo, akieleza kuwa hatua hiyo ni kielelezo cha uongozi bora na wenye kuacha alama chanya katika taasisi.**

## WATUMISHI BORA, WA MUDA MREFU WAPONGEZWA ISW



Mkuu wa Chuo ISW, Dkt. Joyce Nyoni akizungumza na Watumishi wa ISW katika hafla ya kutambua Wafanyakazi bora na mafunzo yaliyotolewa kwa Watumishi wa ISW, Dar es Salaam, Mei 15, 2026.


**Na Mwandishi wetu**

**MENEJIMENTI ya Chuo cha Ustawi wa Jamii (ISW), imewatambua watumishi walioibuka watumishi bora kwa mwaka 2025, pamoja na walioitumikia taasisi kwa zaidi ya miaka mitano, kwa kuwapa vyeti na mkono wa pongezi.**

**Pongezi hizo zilitolewa Mei 15, 2026 katika halfa iliyoongozwa na Mkuu wa ISW, Dkt. Joyce Nyoni ambaye amewapongeza Watumishi walioibuka bora zaidi katika mwaka 2025.**

**"Kutambua Wafanyakazi hodari ni moja ya motisha ya kuleta chachu ya kufanya kazi kwa bidii zaidi, lakini pia ni sehemu ya wengine kuiga mfano ili kupokezana kijiti hiki cha kuwa Mfanyakazi bora," amesema Dkt. Joyce.**

**“Kwa Watumishi wote, naomba niwapongeze sana na kuwashukuru kwa kuwa sehemu ya mafanikio ya taasisi yetu, na niwaombe muendelee kuchapa kazi,"amesema.**



Pichani ni Watumishi wa ISW kati ya waliohudhuria mafunzo kuhusu masuala ya usalama mahali pa kazi iliyofanyika kampasi ya Dar es Salaam, Mei 15, 2026.

**Aidha, amesema Watumishi wa ISW katika hafla hiyo walipata mafunzo kutoka kwa wataalam kutoka Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF) na wakala wa Usalama na Afya Mahali pa kazi (OSHA) kuhusu masuala ya usalama mahala pa kazi, mbinu za kuhakikisha wanakuwa salama katika maeneo ya kazi, pamoja na mafao ya wafanyakazi pale wanapopata ajali au kuumia kazini.**



Mkuu wa Chuo ISW, Dkt. Joyce Nyoni akimkabidhi cheti cha pongezi Mfanyakazi Bora wa Mwaka 2025/2026 Lulu Makata. Katikati ni Naibu Mkuu wa Taasisi, Taaluma Prof. Sotco Komba



Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Mhe. Dkt. Dorothy Gwajima (kulia) akipokea Tuzo Maalum ya Kutambua Uongozi wa Kuigwa Katika Kuendeleza Haki za Kijinsia, Uwezeshaji wa Jamii na Ustawi wa Makundi yaliyo katika Mazingira Hatarishi nchini Tanzania, Tuzo hiyo ilikabidhiwa na Mkuu wa Chuo ISW Dkt. Joyce Nyoni katika Kongamano uwezeshaji watu na ustawi wa jamii , lililofanyika Dar es Salaam, Juni 5, 2026.

# KONGAMANO LA KIMATAIFA LA UWEZESHAJI WATU, USTAWI LAFANA

**Na Mwandishi wetu**

Chuo cha Ustawi wa Jamii (ISW) kimekamilisha kwa mafanikio Kongamano la Kwanza la Kimataifa la Uwezeshaji wa Watu na Ustawi.

Tukio hilo la kihistoria lilifanyika tarehe 5 Juni 2026 katika Ukumbi wa Mikutano wa Kimataifa wa Julius Nyerere (JNICC). Likiongozwa na kauli mbiu "Kuwezesha Watu na Kubadilisha Jamii: Njia za Ustawi Endelevu," kongamano hilo lilifunguliwa rasmi na Mgeni Rasmi, Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Mhe. Dkt. Dorothy Gwajima.

Mkutano huo ulijumuisha uwasilishaji wa mada na mijadala kutoka kwa wasomi, watafiti, watunga sera, na wadau wa maendeleo kutoka zaidi ya nchi 11 duniani.

Akizungumza kuhusu kongamano hilo, Mkuu wa Chuo cha Ustawi wa Jamii (ISW), Dkt. Joyce Nyoni amesema ushiriki huu mpana wa kimataifa ulileta pamoja wataalamu mashuhuri, wakiwemo wasomi kutoka mataifa kama Hungary, Uganda, Norway, Nigeria, na Namibia.

“Kufanyika kwa kongamano hili kumeleta manufaa makubwa kwa ISW kwa kukiongezea hadhi ya kitaaluma na kukiweka katika ramani ya dunia ya taasisi zinazoongoza katika tafiti za kijamii,”amesema Dkt. Joyce.

Aidha, amesema suluhisho na mikakati iliyojadiliwa inatarajiwa kusaidia watunga sera kuunda mbinu bora za kulinda makundi yaliyo katika mazingira magumu, kupunguza umaskini, na kuinua viwango vya maisha vya wananchi.



Prof. Blanka Storen-Vaczy kutoka Norway akiwasilisha mada katika Kongamano la Kimataifa la Uwezeshaji watu na Ustawi, JNICC Dar es Salaam, Juni 5, 2026.

Dkt. Joyce amesema kongamano hilo limeacha alama muhimu katika sekta ya ustawi wa jamii nchini na kimataifa, likithibitisha kuwa uwezeshaji wa wananchi ndio msingi wa mabadiliko endelevu.

Maazimio yaliyofikiwa wakati wa kufunga tukio hili yanatarajiwa kufanyiwa kazi na wadau mbalimbali, ili kubadili nadharia zilizojadiliwa kuwa vitendo vyenye tija kwa maendeleo ya taifa.




**SCAN HAPA KUONA TANGAZO LA MAOMBI YA KUJIUNGA NA KOZI YA UZAMILI KIDIJITALI**

# ISW KUANZA KUDAHILI KOZI ZA MASAFA (ONLINE PROGRAMS) MWAKA WA MASOMO 2026/2027

**Na Mwandishi wetu**

Chuo cha Ustawi wa Jamii (ISW) kinaanza kudahili programu mpya za uzamili kwa mfumo wa masafa na mseto katika mwaka wa masomo wa 2026/2027.

Akizungumza kuhusu program hizo, Mkurugenzi wa Taaluma wa ISW, Dkt. William Manyama amesema hatua hiyo ya kimkakati inalenga kupanua wigo wa utoaji elimu ya juu nchini kwa kutumia teknolojia ya kidijitali, ambapo katika utekelezaji chuo kimetambulisha kozi tatu kuu za uzamili ambazo ni; Shahada ya uzamili wa Ustawi wa Jamii, Shahada ya Uzamili wa Usimamizi wa kimkakati wa Rasilimali Watu na Shahada ya Uzamili wa Sheria za Kazi, Upatanishi na Usuluhishi.

"Kuanzishwa kwa kozi hizo kutaleta manufaa makubwa kwa wanafunzi, kwa kuwa kutawawezesha kusoma kwa urahisi bila kulazimika kuacha ajira au majukumu yao ya kifamilia,"amesema.

Aidha, amesema mfumo huo wa masomo kwa njia ya masafa utapunguza kwa kiasi kikubwa gharama za usafiri na malazi, huku ukiwapa fursa ya kupata elimu bora kutoka mahali popote walipo duniani kupitia majukwaa ya kisasa ya kujifunzia ya mtandaoni. Kwa upande wa chuo, mpango huu utaleta mageuzi kwa kuongeza idadi ya wanafunzi wanaodahiliwa kupata elimu chuoni humo na hivyo kuongeza hadhi ya ISW kitaifa na kimataifa kwa kuwafikia watu wengi zaidi wenye kuhitaji kujiendeleza kielimu.

Aidha, amesema hatua hiyo pia itaongeza mapato kwa chuo na hivyo kusaidia shughuli za uendeshaji, hivyo kuboresha shughuli za kiutafiti zenye manufaa endelevu kitaaluma na jamii kwa ujumla.

"Matokeo ya kuanzishwa kwa programu hizi yatakuwa chanya na ya muda mrefu, yakitarajiwa kuzalisha wataalamu wengi zaidi wenye ujuzi wa hali ya juu katika sekta za ustawi wa jamii na usimamizi wa rasilimali watu kwa kasi kubwa,"amesema na kuongeza:
"Ongezeko hili la wataalamu litachangia moja kwa moja katika kutatua changamoto za kijamii na migogoro ya kikazi maofisini, na hivyo kuchochea tija na maendeleo ya kiuchumi nchini."

# HABARI KATIKA PICHA



Mkuu wa Chuo cha Ustawi wa Jamii Dkt. Joyce Nyoni akiwa bungeni Dodoma akishuhudia tukio la uwasilishwaji wa makadirio ya bajeti ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum kwa Mwaka wa fedha 2026/2027, Dodoma, Juni 1, 2026.




Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya CRDB, Dkt. Abdulmajid Nsekela akipata maelezo ya kozi ya malezi, makuzi na maendeleo ya awali ya mtoto kutoka kwa mhadhiri msaidizi Deusderio Fortunatus alipotembelea banda la Chuo cha Ustawi wa Jamii-ISW katika Maonesho ya Wiki ya Utumishi wa Umma yaliyofanyika Dodoma, Juni 19, 2026.




Mkurugenzi Mtendaji wa Nactvet Dkt. Mwajuma Lingwanda akipata maelezo ya huduma zinazotolewa kutoka kwa wahadhiri wa ISW alipotembelea banda la Chuo cha Ustawi wa Jamii- ISW katika Maonesho ya Biashara ya Kimataifa ya Sabasaba yaliyofanyika Dar es Salaam, Julai 6, 2026

# HABARI KATIKA PICHA



Mratibu wa E-Mrejesho na Dawati la Jinsia Mhadhiri Msaidizi Elizabeth Mashishanga pamoja na Afisa Tehama Mwandamizi Ibrahim Wagala kutoka Chuo cha Ustawi wa Jamii wakiwa katika mafunzo namna ya kushughulikia malalamiko kupitia mfumo wa E-Mrejesho, Dodoma, Juni 02, 2026.




Watumishi wa ISW Kampasi ya Dar es Salaam washiriki maadhimisho ya Siku ya Wafanyakazi Duniani (Meimosi), Dar es Saalam, Mei 01, 2026.




Watumishi wa ISW Kampasi ya Kisangara, Mwanga Kilimanjaro washiriki maadhimisho ya Siku ya Wafanyakazi Duniani (Meimosi), Kilimanjaro, Mei 01, 2026.

# TUFUATILIE KUPITIA MITANDAO YA KIJAMII

isw_official_Tz

chuochaustawiwajamii

taasisiyaustawi

www.isw.ac.tz

0677111200

0735509090 (DSM)
0716121096 (Kisangara)

info@isw.ac.tz